JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS**

**MAENDELEO YA VIJANA**

# MWONGOZO WA UTOAJI MIKOPO KUPITIA PROGRAMU YA KITAIFA YA UWEZESHAJI VIJANA KIUCHUMI

**APRILI, 2026**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**MAENDELEO YA VIJANA**

# MWONGOZO WA UTOAJI MIKOPO KUPITIA PROGRAMU YA KITAIFA YA UWEZESHAJI VIJANA KIUCHUMI

**APRILI, 2026**

# YALIYOMO

**VIFUPISHO VYA MANENO** ........................................ iv

**FASILI YA MANENO** ........................................ v

**MAELEZO YA WAZIRI WA NCHI** ........................................ vii

**DIBAJI** ........................................ viii

**SURA YA KWANZA : UTANGULIZI** ........................................ 1

1.1 Usuli ........................................ 1

1.2 Malengo ya Mwongozo ........................................ 2

1.3 Umuhimu wa Mwongozo ........................................ 2

**SURA YA PILI : UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA KITAIFA YA UWEZESHAJI VIJANA KIUCHUMI** ........................................ 3

2.1. Vyanzo vya Fedha ........................................ 3

2.2. Usimamizi wa Fedha ........................................ 3

2.3. Maeneo ya Kipaumbele ........................................ 3

2.4. Vigezo vilivyotumika kuweka Vipaumbele ........................................ 4

2.5. Walengwa wa Mkopo ........................................ 4

2.6. Sifa za Mwombaji ........................................ 4

2.7. Muda, Kiwango na Riba ya Mkopo ........................................ 5

2.8. Utaratibu wa kuwapata Wanufaika ........................................ 5

2.9. Kujenga uwezo kwa Wanufaika ........................................ 5

2.10. Utoaji na Urejeshaji wa Mikopo ........................................ 6

2.10.1. Utoaji wa Mikopo ........................................ 6

2.10.2. Urejeshaji wa mikopo ........................................ 6

2.11. Viambatisho vya Maombi ya Mkopo ........................................ 6

**SURA YA TATU: MATOKEO** ........................................ 8

3.1 Matokeo Tarajiwa ........................................ 8

3.2 Mikakati ya kufikia malengo ........................................ 8

3.4 Muda wa uchambuzi wa Maombi ya Mkopo ........................................ 9

**SURA YA NNE: MGAWANYO WA MAJUKUMU** ........................................ 10

4.1 Utangulizi ........................................ 10

4.2 Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana ........................................ 10

4.3 Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu)................................ 11
4.4 Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI ........................................................................................ 11
4.5 Wizara ya Fedha ........................................................................................................................ 12
4.6 Wizara za Kisekta......................................................................................................................... 12
4.7 Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa .........................................12
4.8 Taasisi za Fedha ........................................................................................................................ 13
4.9 Majukumu ya Timu Wataalamu Anuai .................................................................................. 13
4.10 Vijana ....................................................................................................................................... 13

**SURA YA TANO: MAWASILIANO KWA UMMA ...................................................... 14**
5.1 Utangulizi .................................................................................................................................... 14
5.2 Mpango wa Mawasiliano kwa Umma....................................................................................... 14
5.3 Mfumo wa Mawasiliano na Wadau.......................................................................................... 15
5.3.1 Ngazi ya Kitaifa ...................................................................................................... 15
5.3.2 Ngazi ya Mkoa ...................................................................................................... 15
5.3.3 Ngazi ya Wilaya.......................................................................................................... 15
5.3.4 Ngazi ya Halmashauri .............................................................................................. 15

**SURA YA SITA: UFUATILIAJI NA TATHMINI ........................................................... 16**
6.1 Utangulizi .................................................................................................................................... 16
6.2 Ufuatiliaji....................................................................................................................................... 16
6.3 Tathmini ...................................................................................................................................... 16
6.4 Viashiria vya Utendaji ................................................................................................................ 17
6.5 Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji .............................................................................................. 17
6.6 Hitimisho .................................................................................................................................... 18
VIAMBATISHO.......................................................................................................................19
Kiambatisho Na.1: Mchanganuo wa Matumizi ya Shilingi Bilioni 200 ...............................19
Kiambatisho Na.2: Kalenda ya Kupokea Fedha kutoka Wizara ya Fedha ......................19
Kiambatisho Na.3: Viashiria ...................................................................................20

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| BBT | Building a Better Tomorrow |
| BRELA | Business Registrations and Licensing Agency |
| NIDA | National Identification Authority |
| OR-MV | Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana |
| OWM-TAMISEMI | Ofisi ya Waziri Mkuu -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TIN | Taxpayer Identification Number |
| YDF | Youth Development Fund |

# FASILI YA MANENO

| | |
|---|---|
| Kijana | Mtu binafsi wa kike au wa kiume mwenye umri kuanzia miaka 18 hadi 35 kwa mujibu wa Mwongozo huu. |
| Kampuni Changa | Kampuni yoyote ya kijana yenye wazo la kutekeleza shughuli za kiuchumi. |
| Biashara Changa | Biashara yoyote ya kijana inayoanza kutekeleza shughuli za kiuchumi. |
| Uwezeshaji wa Vijana | Juhudi za makusudi zinazotekelezwa na Serikali na Sekta Binafsi ili kuwasaidia vijana kushiriki katika shughuli za kiuchumi kupitia sera, sheria, mikakati, programu na huduma za uwezeshaji. |
| Shughuli za Kiuchumi | Shughuli zote za uzalishaji, usambazaji, uongezaji thamani, ununuzi na uuzaji wa bidhaa na utoaji huduma zinazofanywa na vijana katika sekta mbalimbali. |
| Ujuzi | Ujuzi maalum wa kiufundi kulingana na taaluma za sekta husika na ujuzi tepe (uwezo wa kuwasiliana, kujiamini, ubunifu, uaminifu, uadilifu, uwajibikaji,uzalendo, uwezo wa kuongoza, kutumia nadharia kwa vitendo na kuwa na mtazamo chanya kufanya kazi kwa ubia). |
| Ubunifu | Mchakato wa kutafsiri wazo au ugunduzi kuwa bidhaa au huduma ambayo inajenga thamani ambayo wateja wanaweza kuwa tayari kugharimia. Inaweza kuwa katika mfumo wa bidhaa au huduma mpya au iliyoboreshwa, au kuwa katika mpangilio mpya au ulioboreshwa. |
| Uongezaji Thamani | Mchakato wa kubadilisha malighafi au bidhaa ghafi kuwa bidhaa iliyokamilika au yenye ubora wa juu zaidi ili kuongeza thamani yake sokoni, sifa na matumizi. |
| Mnufaika | Kijana, kikundi, biashara au kampuni iliyopokea na kutumia fedha zilizokopwa kutoka kwenye taasisi ya fedha kupitia Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi. |

| | |
|---|---|
| Mkopaji | Kijana, kikundi, biashara au kampuni iliyokopa fedha taslimu au vifaa kutoka kwa mkopeshaji kwa makubaliano ya kurejesha kwa riba ndani ya muda maalum. |
| Mkopeshaji | Taasisi ya fedha iliyoingia makubaliano na OR-MV kwa ajili ya kutoa mikopo kwa makubaliano ya kurejesha kwa riba ndani ya muda maalum. |
| Taasisi ya Fedha | Benki au Taasisi Ndogo za Fedha itakayoingia makubaliano na OR-MV kwa lengo la kutoa mikopo kwa vijana. |

# MAELEZO YA WAZIRI WA NCHI



Vijana ni rasilimali na nguvu muhimu kwa maendeleo ya Taifa. Kwa mujibu wa Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 inaonesha, vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35 ni takribani milioni 21, sawa na asilimia 34.4 ya idadi ya watu wote. Aidha, kwa mujibu wa tafiti wa nguvu kazi vijana wanachangia zaidi ya asilimia 55 ya nguvu kazi ya Taifa. Ukubwa wa kundi hili na umuhimu wake katika ujenzi wa Taifa ni sababu tosha ya kututafakarisha kama Taifa juu ya kuandaa mipango madhubuti ya kuwawezeshaji vijana ili kukabiliana na changamoto ya ajira inayowakabili vijana wetu kwa sasa.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuwawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana mwaka 1993 na kutunga Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007, toleo la mwaka 2024. Pamoja na jitihada zilizochukuliwa, bado kuna changamoto zinazowakabili vijana hasa ukosefu wa mikopo yenye gharama na masharti nafuu.

Kwa kutambua hilo, tarehe 14 Novemba 2025 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kufungua rasmi Bunge La 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jijini Dodoma, alionesha dhamira ya dhati ya Serikali kuwawezesha vijana kwa kutenga shilingi bilioni 200 kupitia Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi ili kuongeza upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu.

Ili kuleta ufanisi wa Programu husika, Serikali imeendaa Mwongozo wa Utoaji wa Mikopo kupitia Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi. Mafanikio ya utekelezaji wa Mwongozo huu yanategemea juhudi za makusudi za kuwawezesha vijana kupata mikopo yenye masharti nafuu na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi.

Hivyo, nitoe rai kwa taasisi husika kuanzia ngazi ya Taifa hadi Halmashauri kuimarisha utendaji na kuwezesha huduma stahiki kwa kundi la vijana lililokusudiwa. Aidha, ninahimiza taasisi kutumia Mwongozo huu kwa lengo la kuchochea ushiriki wa vijana katika shughuli za kiuchumi nchini.



**Dkt. Joel Arthur Nanauka (Mb.)**
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MAENDELEO YA VIJANA**

# DIBAJI



Serikali inatekeleza Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi ili kuchochea ushiriki wa vijana kwenye shughuli za kiuchumi. Katika kutekeleza Programu hii kwa ufanisi, Serikali imeandaa Mwongozo wa utoaji wa Mikopo kupitia Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi ambao unalenga kuweka utaratibu wa usimamizi na utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi ili kuongeza fursa za ajira na mchango wa vijana katika maendeleo ya Taifa.

Mwongozo umeelekeza masuala muhimu ya kufuatwa wakati wa kuwawezesha vijana kiuchumi kupitia Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi. Pia, Mwongozo umebainisha walengwa wa programu, malengo ya programu, sifa za wanufaika, taratibu za utoaji na urejeshaji wa mikopo, na majukumu ya wadau muhimu kuanzia ngazi ya Wizara za kisekta, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, taasisi za fedha na vijana.

Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, inatoa shukrani za dhati kwa wadau mbalimbali ambao kwa namna moja au nyingine wameshiriki kikamilifu katika kufanikisha maandalizi ya Mwongozo huu. Wadau hao ni Wizara za Kisekta, Taasisi za Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Ni matarajio yangu kuwa, Mwongozo huu utarahisisha uratibu wa utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana na utakuwa chachu ya kuongeza ajira kwa vijana.

Natoa rai kwa wadau wote wanaohusika na utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi kuuelewa na kuutumia ipasavyo Mwongozo huu ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi.

Jenifa C. Omolo
**KATIBU MKUU**
**OFISI YA RAIS MAENDELEO YA VIJANA**

# SURA YA KWANZA:

## UTANGULIZI

### 1.1 Usuli

Vijana katika nchi yoyote duniani ni rasilimali watu muhimu kwa maendeleo na chachu ya mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia. Vilevile, ni rasilimali inayochangia maendeleo ya Taifa na ni mtaji uliokusanywa wakati wa ujana balehe. Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 zinaonesha kuwa takribani asilimia 34.4 ya Watanzania wana umri kati ya miaka 15 na 35. Vilevile, Tafiti ya Nguvu Kazi (2021) inabainisha kuwa takribani asilimia 55.6 ya nguvu kazi inatokana na kundi la vijana. Kutokana na takwimu, vijana ni miongoni mwa nguzo na rasilimali muhimu kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuwawezesha vijana kiuchumi ikiwemo kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF) chini ya Sheria ya Fedha (The Exchequer and Audit Ordinance, Cap 439) Na. 21 ya mwaka 1961 kifungu cha 17 (1) mwaka 1993, kutunga kwa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007, toleo la mwaka 2024, mikopo ya vijana kupitia programu ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri, Programu ya Kukuza Ujuzi kwa Vijana na Programu ya Jenga Kesho Iliyobora (BBT). Lengo kuu la jitihada hizi ni kuwawezesha vijana kukuza ujuzi na kupata mitaji kwa njia ya mikopo yenye gharama na masharti nafuu ili waweze kuanzisha au kuendeleza miradi ya uzalishaji mali katika mfumo wa kibiashara. Kupitia jitihada hizi, vijana hujengewa uwezo wa kujitegemea, kuongeza fursa za ajira na kuchochea ushiriki katika shughuli za kiuchumi kwa lengo la kupunguza umasikini.

Pamoja na jitihada zilizofanyika vijana wameendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo: U**finyu wa nafasi za ajira** ukilinganisha na ongezeko la vijana katika soko la ajira. Inakadiriwa zaidi ya asilimia 75 ya nguvu kazi ya vijana hawana ajira rasmi; **Kutokidhi vigezo vya mikopo** vilivyowekwa na taasisi za fedha. Takwimu zinaonesha zaidi ya asilimia 80 ya vijana hawakidhi vigezo vya kupata mikopo vilivyowekwa na taasisi za fedha ukilinganisha na asilimia 20 ya watu wenye umri zaidi ya miaka 35; na **ufinyu wa fursa za mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana**. Takwimu zinaonesha kuwa wastani wa asilimia 80 ya watu wanaopatiwa mafunzo ya ujuzi wa ujasiriamali wana umri zaidi ya miaka 40 kundi ambalo ni chini ya asilimia 30 ya Watanzania wote.

Ili kukabiliana na changamoto zilizoainishwa, Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2025-2030, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 na Sera ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka

2007, toleo 2024 zinaelekeza kuwa uwezeshaji wa vijana kiuchumi ni miongoni mwa nguzo muhimu kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu. Katika kutekeleza dhamira ya kuwawezesha Vijana, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kufungua rasmi Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jijini Dodoma, aliahidi kutenga shilingi bilioni 200 ili kuongeza upatikanaji wa mikopo yenye gharama na masharti nafuu kwa vijana. Katika kutekeleza ahadi hiyo, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana imeandaa Mwongozo wa Utoaji Mikopo kupitia Programu ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi.

## 1.2 Malengo ya Mwongozo

Lengo kuu la Mwongozo ni kuweka utaratibu wa usimamizi na utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi ili kuongeza fursa za ajira na mchango wa vijana katika maendeleo ya Taifa. Malengo mahsusi ni:-

(i) Kuongeza ufanisi wa utoaji wa mikopo kwa vijana;
(ii) Kuainisha maeneo ya kimkakati yatakayozingatiwa katika utoaji wa mikopo;
(iii) Kubainisha walengwa wa mikopo na utaratibu utakaotumika kuwapata;
(iv) Kubainisha majukumu na wajibu wa kila sekta; na
(v) Kuainisha taratibu za ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za utoaji na urejeshaji wa mikopo.

## 1.3 Umuhimu wa Mwongozo

(i) Mwongozo utasaidia kuboresha uratibu na usimamizi wa Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi;

(ii) Kuweka uelewa wa pamoja kuwa fedha zinazotolewa kupitia Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi ni mkopo na sio ruzuku;

(iii) Kubainisha kwa uwazi kwamba fedha ya mkopo ni ya mzunguko (Revolving Fund) hivyo ni sharti irejeshwe katika Mfuko wa Maendeelo ya Vijana; na

(iv) Kubainisha utaratibu utakaotumika kwa ajili ya vijana kupata mikopo husika.

# SURA YA PILI:

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA KITAIFA YA UWEZESHAJI VIJANA KIUCHUMI

### 2.1. Vyanzo vya Fedha

Vyanzo vikuu vya fedha kwa Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi ni:-

(i) Mfuko Mkuu wa Serikali;
(ii) Riba ya asilimia ya mkopo inayotozwa kwa wanufaika;
(iii) Fedha kutoka wabia wa maendeleo katika sekta mbalimbali;
(iv) Kiasi cha fedha kitachokopeshwa kutokana na uwiano na fedha iliyowekwa (exposure ratio); na
(v) Vyanzo vingine halali vya mapato kwa kadri itakavyoamuliwa na Mamlaka.

### 2.2. Usimamizi wa Fedha

Fedha za Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi zitawekwa na kurejeshwa katika Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kupitia Akaunti Na.01J10227640000 Benki ya CRDB, Tawi la Azikiwe.

### 2.3. Maeneo ya Kipaumbele

Mwongozo unabainisha maeneo ya kipaumbele kwa kuzingatia Maeneo ya kimkakati (*Strategic areas*). Maeneo hayo ni:-

(i) Viwanda (25%);
(ii) Uvuvi na Mifugo (18.5%);
(iii) Kilimo (15%);
(iv) Maeneo Mtambuka (14.5%);
(v) Taasisi Ndogo za Fedha Zinazokopesha Vijana (5.5%)
(vi) Madini (5%)
(vii) Biashara/Kampuni Changa (Start-Ups) (5%);
(viii) Bunifu na Gunduzi (5%);
(ix) Sanaa na Michezo (2.5%);
(x) Biashara Ndogo Ndogo (2.5%); na
(xi) Mafunzo na usimamizi (1.5%).

## 2.4. Vigezo vilivyotumika kuweka Vipaumbele

Katika Mwongozo huu, vigezo vilivyotumika kuweka vipaumbele ni:-

(i) **Maeneo yenye matokeo makubwa:** maeneo yatakayohusika ni yale yatakayoleta matokeo makubwa, kwa muda mfupi na muda mrefu na kuwagusa vijana wengi kwa wakati mmoja;

(ii) **Kuzalisha ajira kwa wingi:** Maeneo ya kipaumbele yawe na uwezo wa kuzalisha ajira yenyewe na kuchochea uzalishaji wa ajira katika maeneo mengine;

(iii) **Kuongeza thamani:** Kipaumbele kitaelekezwa kwenye maeneo ambayo yanatoa fursa katika uzalishaji wa malighafi na uongezaji thamani; na

(iv) **Fursa ya kukua na uendelevu:** maeneo ya kipaumbele yawe na uwezo wa kukua yenyewe na kuchochea ukuaji wa maeneo mengine; na

(v) **Kuongeza mapato ya Serikali:** maeneo yawe na uwezo wa kuzalisha na kukuza vyanzo vya mapato kwa wingi na kwa muda mrefu.

## 2.5. Walengwa wa Mkopo

Programu hii inalenga kuwawezesha biashara zinazoanza au zinazoendelea kwa:-

(i) Vijana binafsi wa kike na wa kiume wanaojishughulisha na shughuli za kiuchumi,

(ii) Vikundi vya vijana vilivyosajiliwa na vinavyojishughulisha na shughuli za kiuchumi; na

(iii) Kampuni na Biashara/Kampuni Changa (start - ups) zinazoendeshwa na vijana.

## 2.6. Sifa za Mwombaji

Sifa zinazohitajika kwa waombaji wenye nia ya kupata mkopo:-

(i) Awe ni raia wa Tanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 mpaka 35;

(ii) Awe na biashara inayotambuliwa na Mamlaka katika eneo husika kwa biashara inayoendelea;

(iii) Awe na nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au Namba ya NIDA;

(iv) Awe na andiko la mradi / biashara inayoombewa mkopo;

(v) Awe na historia nzuri ya urejeshaji wa mikopo kwa aliyewahi kukopa;

(vi) Asiwe mwajiriwa wa Serikali au Taasisi za Sekta Binafsi; na

(vii) Awe na akaunti ya benki na namba ya simu iliyosajiliwa kwa jina la mwombaji.

## 2.7. Muda, Kiwango na Riba ya Mkopo

Katika kutekeleza Mwongozo huu, wadau watazingatia muda, viwango vya mkopo na riba iliyokubaliwa katika utoaji mikopo kwa vijana.

(i) **Muda wa mkopo**: muda wa mkopo ni kuanzia miezi sita (6) hadi miezi 36 na itategemea aina ya biashara ambayo Mwombaji ameombea mkopo;

(ii) **Muda wa matazamiao:** Kutakuwa na muda wa matazamio ambao utategemea aina ya shughuli ya kiuchumi iliyoombewa mkopo kulingana na mkataba;

(iii) **Riba ya mkopo:** Kutakuwa na riba ya mkopo isiyozidi asilimia tano (5) ya fedha ya mkopo, itakayojumuisha gharama za bima, huduma za kibenki na kukuza mtaji wa mfuko wa Maendeleo ya Vijana; na

(iv) **Ukomo wa Mkopo:** Kiwango cha juu cha ukomo wa mkopo kitakuwa kiasi cha Shilingi 500,000,000.

## 2.8. Utaratibu wa kuwapata Wanufaika

Walengwa wote watapatikana kwa uwazi na kwa ushindani kwa kuzingatia vigezo vya mkopo husika. Aidha, utaratibu na hatua zitazotumika kuwapata wanufaika ni kama ifuatavyo:

(i) Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana itatoa matangazo ya mikopo;

(ii) OR-MV itapokea maombi ya mkopo kutoka kwa waombaji kulingana na aina ya mradi na kuyatenga kisekta;

(iii) Timu ya Wataalam Anuwai itafanya uchambuzi wa maombi yaliyowasilishwa na kupendekeza majina ya waliokidhi vigezo;

(iv) OR-MV itawasilisha orodha ya majina ya waliokidhi vigezo kwenye taasisi za fedha;

(v) Taasisi za fedha zitafanya uhakiki kwa waombaji wanaopendekezwa na kuwasilisha taarifa ya uhakiki kwa OR-MV; na

(vi) OR-MV itatangaza orodha ya wanufaika na kuratibu zoezi la kujenga uwezo kwa vijana.

## 2.9. Kujenga uwezo kwa Wanufaika

OR-MV itaratibu programu maalum ya kuwajengea uwezo wanufaika kabla, wakati na baada ya kupata mikopo. Programu hiyo itahusisha wizara za kisekta, taasisi za fedha na wadau mbalimbali. Pamoja na masuala mengine, vijana watajengewa uwezo kuhusu ujuzi kwa mujibu wa taaluma za sekta husika.

## 2.10. Utoaji na Urejeshaji wa Mikopo

Utaratibu wa utoaji na urejeshaji wa mikopo ya Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi utafanyika kwa kuzingatia taratibu na miongozo ya Taasisi ya Fedha husika iliyoingia makubaliano na Serikali.

### 2.10.1. Utoaji wa Mikopo

Mikopo hii itatolewa kwa kufuata taratibu, miongozo na vigezo vilivyowekwa. Utaratibu wa utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana itafanyika kwa kuzingatia hatua zifuatazo: -

(i) Mnufaika atakidhi taratibu za kisheria za benki husika za kupata mkopo;

(ii) Mnufaika atasaini mkataba na benki; na

(iii) Wanufaika waliokidhi vigezo watawekewa fedha za mikopo kwenye akaunti au kukopeshwa vifaa kulingana na aina ya mkopo walioomba.

### 2.10.2. Urejeshaji wa mikopo

Mikopo yote itakayotolewa kwa vijana itarejeshwa kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa mkopo kati ya Mkopaji ambaye ni Kijana na Mkopeshaji ambaye ni Benki. Urejeshaji na ufuatiliaji wa mikopo utafanyika kwa utaratibu ufuatao:

(i) Urejeshaji wa mikopo utafanyika kulingana na masharti yaliyowekwa kwenye Mkataba wa Mkopo kati ya mkopaji na taasisi za fedha;

(ii) Ratiba na kiwango cha marejesho ya mkopo zitaandaliwa na taasisi za fedha ili kuwawezesha vijana kufahamu riba, muda na kiwango cha marejesho kabla ya kupokea mkopo;

(iii) Marejesho yatafanyika ndani ya muda uliobainishwa katika mkatabawa mkopo; na

(iv) Taasisi za fedha husika zitafuatilia na kuandaa taarifa za utoaji na urejeshaji wa mikopo kwa kila robo mwaka wa fedha na kuziwasilisha katika OR – MV.

## 2.11. Viambatisho vya Maombi ya Mkopo

Maombi ya mkopo yataambatisha nyaraka kulingana na aina ya mkopo katika sekta mbalimbali. Pamoja na viambatisho vya kisekta, vifautavyo vitatakiwa kuwasilishwa na waombaji wote:

(i) Barua ya maombi ya mkopo;

(ii) Andiko la mradi;

(iii) Utambulisho wa Mlipa kodi (TIN) na Leseni ya Biashara kama ipo;

(iv) Vibali na uthibitisho wa usajili kutoka kwenye mamlaka husika kulingana na aina ya biashara;

(v) Barua ya utambulisho wa eneo la biashara kutoka kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa/Kijiji;

(vi) Picha ya pasipoti ya mkopaji zilizopigwa ndani ya muda usiozidi miezi mitatu kabla ya maombi;

(vii) Uthibitisho wa vyanzo vingine vya mapato kama vipo;

viii) Kitambulisho cha Taifa au Namba ya NIDA au Hati ya Kusafiria au Leseni ya Udereva au Kitambulisho cha Mpiga Kura;

(ix) Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka mmoja kwa upande wa kampuni;

(x) Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN), Uthibitisho wa Ulipaji Kodi (*Tax Clearence*) na Katiba *(Memorandum and Article of Associations)* kwa upande wa kampuni;

(xi) Nakala ya Taarifa ya Mwaka (Annual Returns) iliyoidhinishwa na BRELA kwa kampuni kama ipo;

(xii) Muhtasari wa kikao uliosainiwa na wakurugenzi wa kampuni ukioneshamahitaji ya kuomba mkopo;

(xiii) Muhtasari wa kikao uliosainiwa na wanachama wa kikundi wenye ajenda ya maombi ya mkopo; na

(xiv) Nyaraka yoyote itakayohitajika kwa ajili ya kuthibitisha maombi.

# SURA YA TATU:

## MATOKEO

### 3.1 Matokeo Tarajiwa

Utekelezaji wa Mwongozo unatarajia kuleta matokeo yafuatayo ndani ya kipindi cha miaka mitano 2025/26 – 2029/30:-

(i) Viwanda 25 vipya vidogo na vya kati;

(ii) Mashamba 50 mapya ya umwagiliji;

(iii) Vitalu 20 vya uchimbaji mdogo wa madini;

(iv) Vizimba 500 vipya vya ufugaji samaki;

(v) Mikataba 50 ya utoaji huduma na ujenzi;

vi) Bunifu na gunduzi 300 za vijana;

(vii) Jumla ya vijana 15,000,000 watajengewa uwezo wa ujuzi katika masuala ya kiuchumi na kupata mikopo; na

(viii) Jumla ya ajira mpya za moja kwa moja 2,250,000 zitapatikana.

### 3.2 Mikakati ya kufikia malengo

Ili kufikia malengo yaliyokusudiwa, mikakati ifuatayo itazingatiwa na kutekelezwa:-

(i) Wanufaika wote watapatikana kwa utaratibu wa uwazi;

(ii) Kuimarisha mfumo wa uchambuzi wa maombi ya mikopo;

(iii) Kuimarisha mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini;

(iv) Mikopo ya uwekezaji (Capital Expenditure – CAPEX) itatolewa kwa njia ya vifaa (Asset financing), isipokuwa za mtaji wa uendeshaji (Working Capital) zitatolewa kwa njia ya fedha taslimu kupitia benki;

(v) Fedha zitatolewa kwa mfumo wa mkopo kati ya benki na mkopaji, kwa kuzingatia kiwango cha riba kilichokubaliwa katika mkataba na Mwongozo;

(vi) Kutoa usaidizi wa kiufundi katika hatua zote za miradi ya vijana ikiwa ni pamoja na ujuzi wa eneo husika; na

(vii) Ukuaji na uendelevu wa Programu utapewa kipaumbele kwa kushirikiana na benki washirika ili kuhakikisha mikopo iliyotolewa inarejeshwa kwa wakati.

### 3.4 Muda wa uchambuzi wa Maombi ya Mkopo

Muda wa uchambuzi wa maombi ya mkopo utakuwa muda usiozidi **siku 30** za kazi kwa kufuata mtiririko ufuatao:-

(i) Uchakataji wa maombi ya mkopo utakamilika ndani ya siku 14 tokea tarehe ya kupokea maombi; na

(ii) Taasisi za fedha zitatakiwa kukamilisha uhakiki na kutoa fedha kwa wanufaika waliokidhi vigezo ndani siku 14 tokea tarehe ya kupokea orodha ya wanufaika kutoka OR-MV.

# SURA YA NNE:

## MGAWANYO WA MAJUKUMU

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea mgawanyo wa majukumu wa Wizara na taasisi za sekta ya umma na sekta binafsi kwa kuainisha majukumu ya wadau mbalimbali katika utekelezaji wa Mwongozo wa utoaji wa Mikopo kupitia Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi.

### 4.2 Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana

Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana yenye dhamana na vijana itakuwa na jukumu la kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi. Aidha, Ofisi itachukua hatua stahiki zinazohusisha upatikanaji wa rasimali fedha kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa Programu. Katika kutekeleza jukumu hilo, Ofisi itafanya yafuatayo:-

(i) Kuratibu na kusimamia Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi;

(ii) Kuwasilisha maombi na kupokea fedha kutoka Wizara ya Fedha na washirika wa maendeleo kwa ajili ya Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi;

(iii) Kutoa mwongozo wa kisera unaohakikisha utoaji wa mikopo unazingatia mahitaji na fursa za vijana;

(iv) Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Utoaji Mikopo kupitia Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi;

(v) Kuratibu programu maalum ya kuwajengea uwezo wanufaika kabla, wakati na baada ya kupata mikopo;

(vi) Kuratibu utekelezaji wa mikataba ya ushirikiano wa shughuli za wadau wanaohusika na utoaji wa mikopo kwa vijana;

(vii) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utoaji wa mikopo kwa vijana;

(viii) Kuratibu zoezi la tathmini la maombi ya mikopo yanayowasilishwa na vijana;

(ix) Kutangaza orodha ya wanufaika waliokidhi vigezo kwa umma; na

(x) Kuwasilisha orodha ya wanufaika waliokidhi vigezo kwenye taasisi za fedha.

(xi) Kuhamasisha urejeshwaji wa mikopo kwa vijana;

(xii) Kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji; na

(xiii) Kufungamanisha afua za Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi na mipango ka kitaifa.

## 4.3 Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu)

Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) yenye dhamana ya kuratibu uwezeshaji kiuchumi ikiwemo mifuko na programu za uwezeshajhi nchini, itatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuratibu na usimamizi utendaji wa mifuko na programu za uwezeshaji zote;

(ii) Kufuatilia na kutathmini utendaji wa mifuko na programu za uwezeshaji yote nchini; na

(iii) Kuishauri Serikali kuhusu namna bora ya kuongeza ufanisi katika utendaji wa mifuko na programu za uwezeshaji zote; na

(iv) Kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mifuko na programu za uwezeshaji kwa mamlaka mbalimbali.

## 4.4 Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI

Ofisi ya Waziri Mkuu -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) ambayo ni msimamizi na mratibu wa shughuli zote zinazofanyika katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa itasimamia majukumu yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi inatekelezwa kwa ufanisi katika kila Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

(ii) Kuchambua na kujumuisha taarifa za utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi kutoka Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa za robo mwaka, nusu mwaka na za mwaka na kuziwasilisha OR-MV.

## 4.5 Wizara ya Fedha

Wizara ya Fedha yenye dhamana na fedha itatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kutoa fedha za Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi na kuziwazilisha OR- MV;

(ii) Kuhakikisha kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anakagua fedha za Serikali zinazoingia kwenye Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi ili kuangalia kama zinatekeleza majukumu kulingana na malengo ya kuanzishwa kwake; na

(iii) Kufuatilia matumizi ya fedha za Serikali katika Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi.

## 4.6 Wizara za Kisekta

Wizara za Kisekta zinazoshiriki katika utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi zitakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kushiriki katika uchambuzi wa maombi ya walengwa;

(ii) Kushiriki katika kujenga uwezo kwa vijana kuhusu ujuzi wa maeneo ya kisekta;

(iii) Kuhamasisha vijana kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kuomba mikopo;

(iv) Kuhamasisha urejeshwaji wa mikopo ya vijana;

(v) Kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji; na

(vi) Kufangamanisha afua za Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi na mipango ka kitaifa.

## 4.7 Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kwa kuzingatia mwongozo huu, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakuwa na majukumu yafuatayo:-

(i) Kuhakiki na kuthibitisha nyaraka za utambulisho za waombaji;

(ii) Kuhamasisha vijana kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kuomba mikopo;

(iii) Kuhamasisha urejeshwaji wa mikopo ya vijana; na

(iv) Kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji.

## 4.8 Taasisi za Fedha

Taasisi za fedha ni wadau muhimu katika utoaji mikopo kupitia Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi na zitakuwa na majukumu yafuatayo:-

(i) Kupokea orodha na nyaraka za vijana waliokidhi vigezo vya kupatiwa mikopo kutoka OR – MV;
(ii) Kukamilisha uhakiki wa maombi ya mikopo kwa wakati;
(iii) Kuhakikisha fedha za mikopo zinatolewa kwa lengo lililokusudiwa;
(iv) Kuwawezesha vijana kufahamu riba, muda na kiwango cha marejesho kabla ya kupokea mkopo;
(v) Kusaini mikataba ya mikopo na kutoa mkopo kwa vijana;
(vi) Kuhakikisha marejesho yanafanyika ndani ya muda uliobainishwa katika mkataba wa mkopo;
(vii) Kuhakikisha walengwa waliokidhi vigezo wanapata mikopo ndani ya siku 14 baada ya kukamilisha nyaraka za maombi ya mkopo; na
(viii) Kufuatilia na kuandaa taarifa za utoaji na urejeshaji wa mikopo kwa kila robo mwaka wa fedha na kuziwasilisha katika OR – MV.

## 4.9 Majukumu ya Timu Wataalamu Anuai

OR-MV itaunda Timu Wataalamu Anuai ambayo inayojumuisha wataalamu kutoka katika sekta mbalimbali. Timu hiyo itakuwa na majukumu yafuatayo:-

(i) Kupitia na kuhakiki sifa za jumla za mwombaji;
(ii) Kufanya uchambuzi na kupitisha orodha ya majina ya vijana waliokidhi vigezo;
(iii) Kushirikiana na taasisi za fedha kufanya uhakiki kwa waombaji wanaopendekezwa na kuwasilisha taarifa ya uhakiki kwa OR-MV; na
(iv) Kutekeleza majukumu mengine yatakayopangwa na OR-MV.

## 4.10 Vijana

Majukumu ya vijana waliojikita kwenye shughuli za kiuchumi ni kama yafuatayo:-

(i) Kuomba mikopo kwa mujibu wa taratibu zilizobainishwa katika mwongozo huu;
(ii) Kushiriki mafunzo kwa ajili ya kujiongezea ujuzi na maarifa;
(iii) Kutoa taarifa sahihi kuhusu shughuli ya kiuchumi kwa taasisi za fedha na mamlaka nyingine pindi zitakapohitajika;
(iv) Kutumia fedha ya mkopo kwa malengo yaliyokusudiwa;
(v) Kutekeleza shughuli uliyoombea mkopo kwa weledi na tija; na
(vi) Kurejesha mikopo kwa wakati.

# SURA YA TANO:

## MAWASILIANO KWA UMMA

### 5.1 Utangulizi

Mwongozo huu unaweka mfumo wa mawasiliano na wadau utakaozingatia ngazi za utawala za Kitaifa, Mkoa na Wilaya ili kuweka msingi wa namna bora ya mawasiliano ndani ya Serikali, kati ya Serikali na wadau mbalimbali na vijana sambamba na utoaji wa taarifa za ujumla kuhusu Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi. Pia, Sura hii inaeleza Mpango wa mawasiliano kwa umma.

### 5.2 Mpango wa Mawasiliano kwa Umma

Mpango wa Mawasiliano ni muhimu kuhakikisha kuwa wananchi, wadau, viongozi wa Serikali, taasisi za fedha na sekta binafsi wanapata taarifa sahihi na kwa wakati ili kushiriki kikamilifu katika uendelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi. Aidha, Mpango wa Mawasiliano unaweka msingi wa uwazi na ushirikishwaji katika utekelezaji wa Programu. Utekelezaji wa Mpango utawezesha vijana kufahamu fursa na kushiriki, kuongezeka kwa ushiriki wa wadau na Programu kuleta matokeo tarajiwa. Malengo ya mpango wa mawasiliano ni yafuatayo:-

(i) Kuelimisha vijana kuhusu fursa na vigezo vya kupata mkopo;

(ii) Kuhamasisha ushiriki wa vijana kwenye shughuli za kiuchumi;

(iii) Kujenga uelewa sahihi wa utaratibu wa maombi na utekelezaji;

(iv) Kuimarisha uwazi na ushirikishwaji wa wadau katika utekelezaji wa Programu;

(v) Kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu hatua za utekelezaji; na

(vi) Kuratibu mawasiliano baina ya Serikali, wadau na jamii.

Katika kujenga uelewa Mpango wa Mawasiliano utalenga kufikia vijana kwa kutumia mitandao ya kijamii, tovuti, vyombo vya habari kama magazeti, redio na televisioni. Aidha, taarifa za mikopo zitatolewa katika mikutano itakayoratibiwa na Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kupitia Jukwaa la Vijana na Wiki ya Vijana pamoja na viongozi katika ngazi mbalimbali.

## 5.3 Mfumo wa Mawasiliano na Wadau

Mfumo wa mawasiliano katika utekelezaji wa Mwongozo wa utoaji wa Mikopo kupitia Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi utahusisha kuanzia ngazi ya Taifa hadi halmashauri.

### 5.3.1 Ngazi ya Kitaifa

Msemaji Mkuu wa utendaji wa Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi katika ngazi ya Kitaifa atakuwa ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana mwenye dhamana ya kuratibu maendeleo ya vijana nchini.

### 5.3.2 Ngazi ya Mkoa

Mkuu wa Mkoa atakuwa Msemaji Mkuu wa Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi katika ngazi ya Mkoa kwa mujibu wa Mwongozo huu na kwa kuzingatia majukumu yake katika mkoa husika.

### 5.3.3 Ngazi ya Wilaya

Mkuu wa Wilaya atakuwa Msemaji Mkuu wa Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi katika ngazi za Wilaya kwa mujibu wa Mwongozo huu na kwa kuzingatia majukumu yake katika wilaya husika.

### 5.3.4 Ngazi ya Halmashauri

Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa Msemaji Mkuu wa Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi katika ngazi ya Halmashauri kwa mujibu wa Mwongozo huu na kwa kuzingatia majukumu yake katika Halmashauri husika.

# SURA YA SITA:

## UFUATILIAJI NA TATHMINI

### 6.1 Utangulizi

Ili kuhakikisha utekelezaji wa Mwongozo wa utoaji mikopo kwa vijana unatekelezwa kwa ufanisi na matokeo yake yanaendana na malengo yaliyokusudiwa, ni muhimu kuweka mfumo madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini kwa lengo la kukusanya, kuchambua na kutumia taarifa za utekelezaji katika ngazi zote.

### 6.2 Ufuatiliaji

Ufuatiliaji utafanyika na taarifa zitaandaliwa kila robo mwaka kwa ajili ya kubaini changamoto zinazohitaji kurekebishwa mapema wakati wa utekelezaji. Ufuatiliaji utawezesha kuangalia utendaji wa Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi kwa lengo la kuangalia hatua za utekelezaji zilizofikiwa, mikopo iliyotolewa, kuangalia kiasi cha fedha kilichotumika katika utekelezaji wa Programu husika, na kubainisha upungufu na changamoto katika utekelezaji wa Programu.

Zoezi la ufuatiliaji pamoja na mambo mengine litahusisha kutembelea vijana ambao wamepata huduma ikiwa ni pamoja na mikopo yenye gharama na masharti nafuu; kuangalia maendeleo ya miradi ya vijana waliopata mikopo; na kufanya midahalo na vijana.

### 6.3 Tathmini

Tathmini ya utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi itafanyika kila baada ya mwisho wa mwaka ili kupima utekelezaji wa programu kwa kuzingatia vigezo maalumu vya ufanisi, umuhimu, uendelevu na kufungamanisha na afua nyingine na matokeo ya muda mrefu. Tathmini ya utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi itafanyika ili kubaini masuala mbalimbali ikiwemo:-

(i) Kuangalia maendeleo na hali ya uchumi wa vijana baada ya kupata mikopo; na

(ii) Kuangalia ufanisi wa shughuli za utekelezaji wa Programu husika;

(iii) Kubaini iwapo huduma zinazotolewa kwa vijana ni bora au duni; na

(iv) Kubaini mambo yanayofanikisha au kuathiri utendaji wa Programu.

### 6.4 Viashiria vya Utendaji

Ufuatuliaji na Tathmini vitafanyika kwa kupima utekelezaji wa Programu na itaangalia viashiria vifuatavyo:-

(i) Ongezeko la kipato kwa vijana wanufaika wa mkopo;

(ii) Idadi ya vijana waliopata mikopo;

(iii) Kiwango cha mikopo chechefu;

(iv) Idadi ya vijana waliojengewa uwezo;

(v) Idadi ya shughuli za kiuchumi zilizoboreshwa kutokana na programu;

(vi) Thamani ya mikopo iliyotolewa kwa jinsi, kisekta na kimkoa;

(vii) Idadi ya viwanda vipya vidogo na vya kati vya vijana vilivyoanzishwa;

(viii) Idadi ya mashamba mapya ya umwagiliji ya vijana;

(ix) Idadi ya vitalu vya uchimbaji mdogo wa madini vya vijana;

(x) Idadi ya vizimba vipya vya ufugaji samaki vya vijana;

(xi) Idadi ya mikataba ya utoaji huduma na ujenzi inayotekelezwa na vijana;

(xii) Idadi ya bunifu na gunduzi za vijana;

(xiii) Idadi ya vijana watajengewa uwezo wa ujuzi katika masuala ya kiuchumi;

(xiv) Idadi ya ajira za moja kwa moja mpya zilizotengenezwa; na

(xv) Idadi ya ajira zisizo za moja kwa moja zilizotengenezwa.

### 6.5 Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji

Mfumo wa kuandaa na kuwasilisha taarifa za Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi utakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Taasisi ya Fedha husika itaandaa taarifa ya kila robo mwaka, nusu mwaka na mwaka ya utoaji na urejeshwaji wa mikopo na kuiwasilisha Wizara yenye dhamana na Maendeleo ya Vijana kwa hatua zaidi; na

(ii) Muda wa kuwasilisha taarifa hiyo utakuwa ndani ya siku 15 baada ya kukamilika kwa robo mwaka ya utekelezaji.

## 6.6 Hitimisho

Mwongozo huu ni nyenzo muhimu itakayowezesha utoaji wa mikopo yenye gharama na masharti nafuu kwa vijana nchini kupitia taasisi za fedha ili kuleta ufanisi uliokusudiwa na Serikali. Dhamira ya Serikali ni kuhakikisha vijana wanaongeza kipato chao na kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi. Hivyo, ngazi zote za utekelezaji wa Mwongozo huu hazina budi kuhakikisha kuwa walengwa wanapatiwa huduma bora zinazokidhi matarajio ya Serikali.

## Kiambatisho Na.1: Mchanganuo wa Matumizi ya Shilingi Bilioni 200

| NA. | ENEO | ASILIMIA | KIASI |
|---|---|---|---|
| 1 | Viwanda na biashara | 25 | 50,000,000,000 |
| 2 | Mifugo na uvuvi | 18.5 | 37,000,000,000 |
| 3 | Kilimo | 15 | 30,000,000,000 |
| 4 | Maeneo mtambuka | 14.5 | 29,000,000,000 |
| 5 | Taasisi ndogo za fedha zinazokopesha vijana | 5.5 | 11,000,000,000 |
| 6 | Madini | 5 | 10,000,000,000 |
| 7 | Biashara/Kampuni changa | 5 | 10,000,000,000 |
| 8 | Bunifu na Gunduzi | 5 | 10,000,000,000 |
| 9 | Sanaa na michezo | 2.5 | 5,000,000,000 |
| 10 | Biashara ndogondogo | 2.5 | 5,000,000,000 |
| 11 | Mafunzo na usimamizi | 1.5 | 3,000,000,000 |
| | **Jumla** | **100** | **200,000,000,000** |

## Kiambatisho Na.2: Kalenda ya Kupokea Fedha kutoka Wizara ya Fedha

| NA. | ENEO | KIASI | Awamu ya Kwanza Jan-Mach, 2026 | Awamu ya Pili Mach-April, 2026 | Awamu ya Tatu April-Juni, 2026 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Viwanda na Biashara | 50,000,000,000 | 4,000,000,000 | 21,000,000,000 | 25,000,000,000 |
| 2 | Kilimo | 30,000,000,000 | 6,000,000,000 | 20,000,000,000 | 4,000,000,000 |
| 3 | Mifugo na Uvuvi | 37,000,000,000 | 23,685,829,751 | 0 | 13,314,170,249 |
| 4 | Maeneo Mtambuka | 29,000,000,000 | 0 | 8,000,000,000 | 21,000,000,000 |
| 5 | Taasisi ndogo za fedha zinazokopesha vijana | 11,000,000,000 | 0 | 0 | 11,000,000,000 |
| 6 | Madini | 10,000,000,000 | 0 | 0 | 10,000,000,000 |
| 7 | Biashara/Kampuni changa (start up) | 10,000,000,000 | 5,000,000,000 | 0 | 5,000,000,000 |
| 8 | Bunifu na gunduzi | 10,000,000,000 | 0 | 0 | 10,000,000,000 |
| 9 | Sanaa na michezo | 5,000,000,000 | 5,000,000,000 | 0 | 0 |
| 10 | Biashara ndogo ndogo | 5,000,000,000 | 5,000,000,000 | 0 | 0 |
| 11 | Mafunzo na Usimamizi | 3,000,000,000 | 0 | 0 | 3,000,000,000 |
| | **Jumla** | **200,000,000,000** | **48,685,829,751** | **49,000,000,000** | **102,314,170,249** |

## Kiambatisho Na.3: Viashiria

| Na. | Eneo la Kufuatilia | Kiashiria | Chanzo cha Taarifa | Muda wa Kukusanya Takwimu |
|---|---|---|---|---|
| **A: UTOAJI MIKOPO** | | | | |
| 1 | Utoaji wa Mikopo | Idadi ya vijana waliopata mikopo kwa jinsi na mikoa | Taarifa ya robo mwaka | Robo mwaka |
| | | Thamani ya mikopo iliyotolewa kwa jinsi, sekta na mikoa | | |
| 2 | Shughuli za kiuchumi za vijana | Idadi ya shughuli za kiuchumi za vijana zilizoanzishwa kisekta na kimkoa. | Taarifa ya nusu mwaka | Miezi 6 |
| | | Idadi ya viwanda vipya vidogo na vya kati vya vijana vilivyoanzishwa | | |
| | | Idadi ya mashamba mapya ya umwagiliji ya vijana | | |
| | | Idadi ya vitalu vya uchimbaji mdogo wa madini vya vijana | | |
| | | Idadi ya vizimba vipya vya ufugaji samaki vya vijana | | |
| | | Idadi ya mikataba ya utoaji huduma na ujenzi inayotekelezwa na vijana | | |
| | | Idadi ya bunifu na gunduzi za vijana | | |
| | | Idadi ya shughuli za kiuchumi za vijana zilizoanzishwa kimkoa. | | |
| **B: UREJESHAJI MIKOPO** | | | | |
| | Urejeshaji mikopo | Mwenendo wa mikopo chechefu | Taarifa ya robo mwaka | Robo mwaka |
| **C: MATOKEO YA KIUCHUMI** | | | | |
| 1 | Hali ya umaskini | Ongezeko la kipato kwa vijana wanufaika wa mkopo | Tathmini za utendaji wa Programu | Kila baada ya miaka mitatu |
| 2 | Ajira | Idadi ya ajira za moja kwa moja mpya zilizotengenezwa | | |
| | | Idadi ya jira zisizo za moja kwa moja zilizotengenezwa. | | |
| **D: MAFUNZO** | | | | |
| 1 | Mafunzo | Idadi ya vijana watajengewa uwezo wa ujuzi katika masuala ya kiuchumi | Taarifa ya robo mwaka | Robo mwaka |

**Imeandaliwa Na:**
**Ofisi ya Rais-Maendeleo ya Vijana,**
**S.L.P 2255, 9 Barabara ya Waziri Mkuu,**
**41207 DODOMA.**